
Kiswahili

Tuthamini lugha zetu

# Mwongozo wa Masomo ya Biblia

## *Injili ya Marko*





# Mwongozo wa Masomo ya Biblia

# *Injili ya Marko*

**Mark Study Guide**

Translated into Swahili by: Amos Malongo & Flavian Mkupasi

Toleo la Majaribio
Nakala 100
Mwezi wa Sita, 2012

Kimepigwa chapa na;
Habari Maalum Press
SLP 7292
Arusha, Tanzania

**Acknowledgements**:

Original text by Susan Lassalle
and edited by Language Programmes Department staff, ©BTL, 2000

All other illustrations by Copyright © Language Recording Inc (Australia).
Used with permission.

**CONTENTS**

Dibaji

Vidokezo vya msingi

Utangulizi wa Injili ya Marko

Marko 1 Yohana na ujumbe wake (Marko 1:1-11)

Marko 2 Wenye haki na watendadhambi (Marko 2:14-17)

Marko 3 Kumfuata Yesu (Marko 3)

Marko 4 Mfano wa mpanzi (Marko 4:1-20)

Marko 5 Imani katika Yesu (Marko 5:21-43)

Marko 6 Yesu, zaidi ya mwanadamu (Marko 6:45-56)

Marko 7 Yesu na watu wa mataifa (Marko 7:24-30)

Marko 8 Yesu, Kristo anayeteseka (Marko 8:27-38)

Marko 9 Kugeuka sura kwa Yesu (Marko 9:2-13)

Marko 10 Aliye mkuu kuliko wote katika ufalme wa Mungu (Marko 10:32-45)

Marko 11 Kuingia Yerusalemu (Marko 11:1-11)

Marko 12 Amri kuu (Marko 12:28-34)

Marko 13 Yesu atarudi tena (Marko 13:24-37)

Marko 14 Karamu ya Bwana (Marko 14:17-26)

Marko 15 Kusulibiwa kwa Yesu (Marko 15)

Marko 16 Kufufuka kwa Yesu (Marko 16)

## DIBAJI

Lengo la kitabu hiki cha mwongozo ni kukuongoza kuipitia taratibu na kuielewa Injili ya Marko. Katika kila sura utafuatilia mistari michache. Katika Injili ya Marko tunaweza kujifunza mambo maalum kuhusu Mungu, Yesu, watu na maisha. Inaweza pia kukupa mfano wa namna ya kuongoza makundi ya kujisomea Biblia, kwa njia ya; (1) kusoma kitabu toka mwanzo hadi mwisho, (2) kuuliza maswali ya kumsaidia kila mmoja kuelewa ujumbe wa Injili na kisha (3) kuuliza maswali na kujadili namna ya kufuata na kufanya yale ambayo Injili inataka tufanye.

Mafunzo haya ya Biblia yanaweza kutumika kwa njia nyingi:
- Mtu mmoja peke yake – katika kujisomea Biblia
- Watu wawili – katika kusoma Biblia kwa pamoja na kuyajadili maswali
- Vipindi vya Kanisa – kitabu hiki kinaweza kumsaidia kiongozi katika kuongoza kundi kusoma na kujadili Injili ya Marko

## VIDOKEZO MUHIMU

Mapendekezo yafuatayo yatakusadia kukifaidi kitabu hiki..

### Omba
Mwombe Mungu akusaidie kuelewa na kufanya kwa vitendo mambo ambayo unajifunza.

### Soma
Kwanza, soma Injili yote ya Marko ili upate wazo kuu la kitabu. Baada ya hapo, soma mara kadhaa kifungu kilicho andaliwa kwa ajili ya somo. Kadiri unavyo soma zaidi, ndivyo utakavyoelewa zaidi na kugundua thamani wa Neno la Mungu.

### Fikiri na tafakari
Soma kila swali na kulifikiria. Unaweza kujibu karibu maswali yote kutoka katika maandiko ya Biblia. Swali linaweza kuwa na majibu zaidi ya moja.  Vipengele vilivyo andikwa katika maandishi ya *mlalo* vipo kwa ajili ya kufafanua mambo magumu.

### Daftari
Inaweza kuwa msaada ukiandika majibu ya maswali katika daftari, ili majibu yote yawe sehemu moja na uweze kuyatumia muda wowote unapohitaji kufanya hivyo.

### Jadili
Chukua nafasi ambayo itakufanya ujihusishe katika kundi na shirikiana na watu wengine majibu yako.

### Kwa vitendo
Kama ukifanya kwa vitendo yale uliyojifunza, Mungu anaweza kuyafanya upya maisha yako, maisha ya familia yako na maisha ya rafiki zako na pia jumuia nzima. Kwa kila somo kuna maswali ya kutafakari – maswali hayo yatakusaidia kufikiria jinsi ya kutekeleza kila ulichojifunza. Maombi yetu kwa ajili yako ni kwamba ugundue zaidi na zaidi thamani ya Neno la Mungu na kwamba upate zaidi na zaidi uhai kamili alioahidi Yesu (Yohana 7:37-38).

## UTANGULIZI WA INJILI YA MARKO

Inasemekana kwamba Injili hii imeandikwa na John Mark. Yeye alikuwa msafiri-pacha wa mtume Paulo (Matendo 12:25) na binamu wa Barnabas (Kol. 4:10). Alikuwa mtoto wa kiroho wa mtume Petro. Injili hii inatazamwa kama ushuhuda wa moja kwa moja (wa macho), na kwa kawaida hudhaniwa kwamba Petro alikuwa chanzo kikuu cha maandiko ya Marko.

Huenda hadhira ya kwanza iliyodhamiriwa  kwa ujumbe huu ilikua kanisa la Roma. Kanisa hili kimsingi lilijawa na Watu wa Mataifa  (wasio wayahudi), na kwa hiyo misemo na tamaduni zozote za kiyahudi, hufafanuliwa na mwandishi.

Katika Injili zote nne katika Agano Jipya, Injili iliyoandikwa na Marko ndiyo fupi zaidi. Yenyewe hujulikana zaidi kwa tabia zake za kuwa na maelezo ya wazi kuhusu matendo ya Yesu na kumwelezea kama mkuu sana, lakini pia, kama mwana wa Mungu anayeteseka kwa hiari. Alifundisha kwa mamlaka, na mafundisho yake yakaimarishwa na miujiza aliyoifanya.

## MARKO SURA YA 1

## YOHANA NA UJUMBE WAKE (MARKO 1:1-11)

*Soma sura ya kwanza yote ili uweze kuuelewa muktadha (mazingira). Halafu soma tena kuanzia mstari wa 1 mpaka wa 11. Mistari hii itakuwa ndiyo kiini cha somo hili.*

1. Katika mstari wa 4 tunaona jina la mjumbe wa Yesu. Jina lake ni nani?

2. Aliwaambia watu wanapaswa wafanye nini? (mst. 4)

3. Yohana Mbatizaji alisema nini kwa watu wote waliokuja kumsikiliza? Aliongea kuhusu nani? (mst. 7 na 8)

4. Yohana Mbatizaji aliwabatiza watu kwa maji. Je, Yesu angewabatiza kwa njia gani watu? (mst. 8)

5. Je, ni nani ambaye pia aliyebatizwa kama ilivyoandikwa katika mstari wa tisa?

6. Yesu alibatizwa wapi? (mst. 9)

7. Kitu gani kilitokea Yesu alipotoka majini? (mst. 10)

8. Unafikiri dhambi ni nini?

9. Mwishoni mwa mstari wa 5, maandiko yanasema kwamba watu wakaziungama dhambi zao. Kuungama dhambi ni kufanya nini?

*Swali la kutafakari:*

10. Unawezaje kukiri na kutubu dhambi zako?

## MARKO SURA YA 2

## WENYE HAKI NA WATENDADHAMBI (MARKO 2: 14-17)

*Soma sura ya pili yote ili uweze kuuelewa muktadha (mazingira). Halafu soma tena kuanzia mstari wa 14 mpaka wa 17. Mistari hii itakuwa ndiyo kiini cha somo hili.*

1. Kazi ya Lawi ilikuwa nini? (mst. 14)

*Nyakati zile, taifa la Israeli lilitekwa na kuwa chini ya utawala wa Warumi. Kulikuwa na watoza ushuru waliofnaya kazi katika selikari ya kirumi, ambao jukumu lao lilikuwa ni kukusanya ushuru kutoka kwa Wayahudi. Wayahudi waliwachukia sana watoza ushuru hawa, kwani waliamini kwamba walikuwa wakikusanya pesa nyingi zaidi kuliko zile walizokuwa wakizipeleka selikalini, na pia kwa sababu walikuwa wakifanya kazi kwa wapinzani wao, yaani Warumi.*

2. Yesu alimwita Lawi amfuate. Lawi aliitikiaje wito huo?

3. Biblia inasema kwamba Lawi alimwalika Yesu nyumbani kwake kula chakula cha jioni. Nani alikuwa pale katika nyumba ya Lawi? (mst. 15)

*Waandishi na Wafarisayo walikuwa sehemu ya uongozi wa kidini wa jamii ya Wayahudi wakati huo. Viongozi hawa walikuwa na mvuto mkubwa katika jamii, huku wengi wao wakiwa wanafiki wakubwa.*

4. Yesu alitoa jibu gani kwa dhihaka waliyoionesha kwake? (mst. 17)

5. Yesu alikuja kwa ajili ya watu gani? (mst. 17)

6. Ni afadhali kuwa mwenye haki kuliko kuwa mtenda dhambi. Ni nani hasa katika simulizi hili hujiona kuwa ni wenye haki? (mst. 16)
7. Baadhi ya watu wanaweza kujiona kuwa ni wenye haki, lakini kuna mtu ambaye anaweza kuishi pasipo kutenda au kufikiria mabaya?

*Maswali ya kutafakari:*

8. Je, unajiona kuwa ni mwenye haki?

9. Unafikiri bado unapaswa kufanya kazi vizuri na kufuata amri kumi za Mungu ili utakasike kwa ajili ya kuokolewa au kupokelewa na Mungu? Kama ndio kwa nini? Na kama sio ni kwa nini?

10. Kama ingekuwa siyo lazima kufanya matendo mema ili uokolewe, je, bado ungefanya mambo mema, na kwa nini?

*Biblia hufundisha katika sehemu zake nyingi kwamba watu huhesabiwa kuwa ni wenye haki ikiwa tu wanamwamini na kumfuata Yesu. Soma Yohana 6:28-29, Warumi 3:28, Wagalatia 2:16 na Waefeso 2:8-9. Tumeokolewa kwa neema pekee, kwa imani pekee.*

11. Je, uelewa wako kuhusu jambo hili unayabadilishaje maisha yako?

## MARKO SURA YA 3

## KUMFUATA YESU (MARKO 3)

*Soma sura ya 3 yote.*

1. Kwa nini watu hawa walikwenda kwa Yesu? (mst. 8)

2. Kwa nini watu walimsonga Yesu kuelekea kando ya ziwa? (mst. 9-10)

3. Pepo wachafu wanatajwa tena katika mstari wa 11. Pepo wachafu walisema nini walipomwona Yesu? Ni katika mstari wa ngapi katika Injili ya Marko, sura ya 1, ambapo Mungu anaongea mambo haya haya kuhusu Yesu?

4. Katika mistari michache ijayo, Yesu anawachagua wafuasi 12 na anawaita “mitume”. Kwa madhumuni gani matatu Yesu aliwachagua mitume hao 12? (mst. 14-15)

5. Unafikiri ni kwa nini Yesu alitaka mitume wakae naye kwa muda kabla hawajatumwa kwenda kuhubiri na kukemea pepo?

6. Katika sura hii tunaweza kuona namna Yesu na kazi zake alivyopokelewa. Je alipokelewaje? (Tazama kwa mfano, mstari wa 8, 11 na 22.

*Maswali ya kutafakari:*

7. Sura ya tatu inakwisha kwa Yesu kuweka bayana kwamba ndugu zake, dada zake na mama yake hasa walikuwa ni nani? (mstari wa 31 – 34). Hii ina maana gani?

8. Kufuatana na maneno ya Yesu, ni jinsi gani tunaweza kuwa kaka zake au dada zake?

## MARKO SURA YA 4

## MFANO WA MPANZI (MARKO 4:1-20)

*Wakati Yesu alipotaka kuwafundisha watu kuhusu ufalme wa Mungu, mara nyingi alifundisha kwa kutumia mifano. Mfano ni hadithi fupi ya kufundishia somo. Soma sura yote ya nne na halafu usome mstari wa 1-20 tena. Mistari hii ndiyo itakayokuwa kiini cha somo hili.*

1. Katika mistari ya 3 – 8 Yesu aliwaambia mfano uliosisitiza aina za udongo ambao mbegu zilianguka na kumea. Taja aina nne za udongo huo.

*Wanafunzi hawakuelewa maana ya mfano, hivyo Yesu aliwaelezea tena. Maelezo yake ya mfano yanafuata katika mistari ya 13 – 20. Ila kwanza, katika mistari ya 11 – 12 Yesu aliwaambia wafuasi wake kwa nini alifundisha kwa mifano. Yesu alielezea kuwa inawezekana kusikia neno la Mungu na bado usielewe maana halisi lakini wale wote walioamua kumfuata Yesu kama Bwana wao watasaidiwa kuelewa maana iliyopo ndani ya maneno hayo.*

2. Je, mbegu huwakilisha nini? (mst.14)

3. Je, barabara ambayo baadhi ya mbegu zilianguka juu yake huwakilisha nini? Na ndege je, huashiria nini? (mstari wa 4 na wa 5).

4. Ardhi yenye miamba ambamo baadhi ya mbegu zilianguka juu yake huwakilisha nini? (mstari wa 5-6 na 16-17)

5. Miiba ambamo baadhi ya mbegu ziliangukia kati yake, huwakilisha nini? (mstari wa 7 na mstari wa 18-19)

6. Udongo mzuri wenye rutuba ambamo baadhi ya mbegu ziliangukia huwakilisha nini? (mstari wa 8 na mstari wa 20)

7. Inaposemwa kwamba mbegu huzaa matunda, unafikiri neno “matunda” linamaana gani?

*Maswali ya kutafakari:*

8. Ni mambo gani katika maisha yako ambayo yangeweza kukuzuia usilifuate Neno la Mungu?

9. Ungefanya nini kuizuia hali hiyo?

## MARKO SURA YA 5

## IMANI KATIKA YESU (MARKO 5:21-43)

*Soma sura ya 5 yote ili uweze kuuelewa muktadha (mazingira). Halafu soma tena kuanzia mstari wa 21 mpaka wa 43. Mistari hii itakuwa ndiyo kiini cha somo hili.*

1. Baada ya Yesu kumponya mtu mwenye pepo mchafu, yeye pamoja na wanafunzi wake walipanda mashuani na kurudi tena n'gambo ya pili ya ziwa Galilaya. Nani alikutana nao katika pwani? (mst. 21)

2. Mtu huyu alimwomba nini Yesu? (mst. 23).

3. Yesu alikuwa akienda na Yairo nyumbani kwake. Wakiwa njiani, mwanamke mmoja alimjia. Nini ilikuwa shida ya yule mwanamke? (mst. 25-26)

4. Je, yule mwanamke alifanya nini wakati alipokuwa katika kusanyiko lililomfuata Yesu? (mst. 27) Kwa nini alifanya hivyo? (mst. 28)

5. Yesu alisema ni kitu gani kilichosababisha mwanamke huyo apone? (mst. 34)

6. Rejea mistari ya 27-28. Vitu gani pale vilionesha kuwa mwanamke alikuwa na imani katika Yesu?

7. Ujumbe gani ulimjia Yairo wakati Yesu alipokuwa akiongea na mwanamke aliyeponywa? (mst. 35)

8. Yesu alisema nini juu ya habari kwamba binti wa Yairo amekufa? (mst. 36)

9. Yesu alifika nyumbani kwa Yairo, akawaondoa waombolezaji, kisha akaingia chumbani ulikokuwa umelazwa mwili wa yule binti. Yesu alisema nini kwa yule binti? (mst. 41)

*Maswali ya kutafakari:*

10. Yairo pamoja na yule mwanamke, waliishi imani yao kwa vitendo. Ni katika nyakati gani maishani mwako ambapo unahitaji kuiishi imani yako kwa vitendo, badala tu ya kusema kwa mdomo kwamba unaamini pasipo kuonyesha kwa vitendo?

## MARKO SURA YA 6

## YESU, ZAIDI YA MWANADAMU (MARKO 6:45-56)

*Soma sura ya 6 yote ili uweze kuuelewa muktadha (mazingira). Halafu soma tena kuanzia mstari wa 45 mpaka wa 56. Mistari hii itakuwa ndiyo kiini cha somo hili.*

1. Yesu alikuwa amekwishafanya muujiza mwingine punde wa kuwalisha maelfu ya watu kwa kutumia mikate mitano tu na samaki wawili. Baada ya watu wote kula na Yesu kuwatawanya makutano, Yesu aliwaambia wanafunzi wake wafanye nini? (mst. 45)

2. Kisha, Yesu alifanya nini? (mst. 46)

3. Upepo ulivuma na kufanya safari fupi kwa mashua kuwa ngumu kwa wanafunzi. Yesu alipoona hivyo alifanya nini? (mst. 48)

4. Je, wanafunzi katika mashua walifikiri kuwa Yesu ni kitu gani? (mst. 49)

5. Yesu aliwaambia maneno gani wanafunzi ambao walikuwa wamejawa na woga? (mst. 50)

6. Yesu alipopanda katika mashua, kulitokea nini? (mst. 51)

7. Wanafunzi walipokeaje? (mst. 51)

9. Marko anaandika kwamba mioyo ya wanafunzi wa Yesu ilikuwa migumu na kwa hiyo walishindwa kuelewa muujiza wa kulisha kundi kubwa la watu (mst. 52). Ni kitu gani hicho ambacho hawakukielewa?

*Swali la kutafakari*

10. Licha ya kwamba wanafunzi wa Yesu walishuhudia miujiza na uwezo wa Yesu, waliogopa sana pale walipokiona kitu ambacho hawakukitegemea. Unaweza kufikiria hali fulani ambapo unaogopa lakini bado ukawa na uwezo wa kuwa na imani katika uwezo na uwepo wa Yesu? Utawezaje kupambana na hali kama hii mbeleni?

## MARKO SURA YA 7

## YESU NA WATU WA MATAIFA (MARKO 7:24-30)

*Soma sura ya 7 yote ili uweze kuuelewa muktadha (maginzira). Halafu soma tena kuanzia mstari wa 24 mpaka wa 30. Mistari hii itakuwa ndiyo kiini cha somo hili.*

1. Yesu hakupenda mtu yeyote amtambue kule Tiro lakini mwanamke mmoja alisikia kuwa Yesu yuko kule. Mwanamke huyo alifanya nini? (mst. 25)

2. Binti yake alikuwa na tatizo gani? (mst. 25)

3. Mwanamke huyo alimwomba Yesu afanye nini? (mst. 26)

4. Nini lilikuwa jibu la Yesu kwa mwanamke yule? (mst. 27)

*Wakati wa Yesu, Wayahudi waliwachukulia wale wasio Wayahudi kama "mbwa", huku Wayahudi wenyewe wakijiita "watoto wa Abrahamu". Mara kwa mara makabila mbalimbali yalichukiana sana. Yesu anatumia picha hii kuijaribu imani ya yule mwanamke. Je, manamke yule, akiwa si Myahudi, alitegemea msaada kutoka kwa Myahudi?!*

5. Jibu la mwanamke huyu lilionyesha unyenyekevu na imani yake. Anasema nini (mst. 28)? Alimaanisha nini kwa kauli yake hiyo?

6. Yesu alikubali ombi la mwanamke yule kwa sababu majibu yake yalionyesha kwamba alikuwa na imani kubwa.Yesu alifanya nini? (mst. 29)

7. Yesu alikuwa Myahudi, na alikuja kama mwokozi wa Wayahudi. Hata hivyo alimsaidia mwanamke asiye Myahudi. Je, simulizi hili linatufundisha nini kuhusu mpango wa Yesu?

*Swali la kutafakari:*

8. Yesu alikuwa ni mwenye neema na mwenye rehema kwa kila aliyekuja kwake (bilakujali rangi au kabila au ulemavu wa kimwili) kama tu walitambua mahitaji yao. Je, wakati mwingine unakaa mbali na watu kwa sababu tu wao wanatoka kabila lingine au kwa sababu wana baadhi ya magonjwa? Badala ya kufanya hivyo, unaweza kufanya nini kuwaonyesha ukarimu kama Yesu alivyofanya?

## MARKO SURA YA 8
## YESU, KRISTO ANAYETESEKA (MARKO 8:27-38)

*Soma sura ya 8 yote ili uweze kuuelewa muktadha (mazingira) Halafu soma tena kuanzia mstari wa 27 mpaka wa 38. Mistari hii itakuwa ndiyo kiini cha somo hili.*

1. Yesu aliwauliza wanafunzi swali gani? (mst. 27)

2. Kutokana na mstari wa 28, kulikuwa na mkanganyiko kuhusu Yesu ni nani. Watu walisema kuwa Yesu ni nani?

3. Yesu aliuliza swali kwa njia tofauti kwa mara ya pili. Alisema nini? (mst. 29)

4. Petro alijibu nini? (mst. 29)

*Kumbuka, Wayahudi walikuwa wanamsubiri Masiha aje na kuwaokoa kutoka kwa Warumi ambao walikuwa wakiwatawala na kuwakandamiza. Yesu alikuja kuwafundisha watu kuhusu ufalme wa Mungu. Hakuja mara hii kuwa mtawala katika ulimwengu, ingawa watu walifikiri Masiha angekuwa mtawala. Walikuwa na matarajio tofauti kabisa kuhusu Masiha.*

5. Alipokwisha jitambulisha wazi wazi na kujulikana dhahiri kwamba yeye ni Kristo, Yesu alianza kuwafundisha wanafunzi kuhusu nini ambacho kitamtokea. Yesu alisema nini kitatokea kwake? (mst. 31)

6. Nani alimchukua Yesu pembeni na kumkemea? (mst. 32)

7. Kisha Yesu alimkemea Petro. Je, Yesu alisema nini? (mst. 33)

*Hapa, Yesu alimwita Petro 'Shetani' kwa sababu Petro alikuwa akifikiri na kuongea moja kwa moja kinyume na makusudi kamili ya ujio wa Yesu. Hata hivyo, Petro na wanafunzi wengine walipaswa kumwona Yesu kama Masiha anayeteseka kwanza. Kama ilivyokuwa kwa Wayahudi wengi, wanafunzi wa Yesu pia walikuwa na matarajio yenye mtarajio tofauti kidogo kuhusu Masiha.*

8. Baadaye Yesu aliongea kuhusu maana ya kuwa mfuasi wa Yesu. Vitu gani vitatu ambavyo mtu lazima avifanye ili amfuate Yesu? (mst. 34)

*Maswali ya kutafakari:*

9. Nini jibu lako kwa swali ambalo Yesu aliwauliza mitume wake: "Ninyi mwasema Yesu ni nani?" (mst. 29)

*Yesu alipaswa kuteswa ili kutimiza mapenzi ya Mungu. Vivyo hivyo wafuasi wa Yesu lazima wawe tayari kumtii Mungu kwa dhati, hata kama inamaanisha kuteseka.*

10. Ina maana gani kujikana mwenyewe, kubeba msalaba wako na kumfuata Yesu. Unawezaje kufanya hivyo katika maisha yako ya kila siku?

## MARKO SURA YA 9

## KUGEUKA SURA KWA YESU (MARKO 9:2-13)

*Soma sura ya 9 yote ili uweze kuuelewa muktadha (mazingira). Halafu soma tena kuanzia mstari wa 2 mpaka wa 13. Mistari hii itakuwa ndiyo kiini cha somo hili.*

1. Yesu aliwachukua akina nani kwenda nao mlimani? (mst. 2)

2. Mwonekano wa Yesu ulibadilika ghafla. Nini kilitokea katika nguo zake? (mst. 3)

3. Nani pia alitokea na Yesu, akizungumza naye? (mst. 4)

4. Unafahamu nini kuhusu kila mmoja wao?

5. Mungu alisema nini? (mst. 7)

6. Baada ya Mungu kuongea katika wingu, nini kilitokea? (mst. 8)

7. Baada ya wanafunzi na Yesu kushuka toka mlimani, ni kitu gani ambacho Yesu aliwaambia wasifanye? (mst. 9) Lakini Yesu aliweka ukoma wa muda katika ombi lile. Ukoma huo wa muda ulikuwa upi?

8. Wale watatu, Petro, Yakobo na Yohana walianza kujadili Yesu alimaanisha nini alipokuwa akizungumza kuhusu kufufuka kutoka wafu. Walimwuliza Yesu swali. Lilikuwa swali gani? (mst. 11)

*Hawa wanafunzi watatu, wakiwa ni Wayahudi, walijua sana mafundisho na unabii wa Agano la Kale. Walijua kuwa Eliya alitakiwa kurudi tena kutoka kuzimu kabla ya kurudi tena kwa Masiha. Kwa sababu hawakuwa wamesikia kuwa Eliya amerudi tena, walihangaika wakijua kama Yesu ndiye kweli Masiha. Yesu alijibu maswali yao kwa kusema kwamba Eliya ameshakuja tena. Alimaanisha Yohana Mbatizaji. Tunajua hilo kwa sababu Matayo anaweka hili wazi katika kitabu chake (Matayo 17:10 13).*

*Maswali ya kutafakari:*

*Katika aya hii, tumekumbushwa kuhusu utakatifu na utukufu wa ajabu wa Mungu. Wanafunzi wa Yesu walipomwona Yesu katika utakatifu na utukufu wake, walitaka kuwa naye, lakini pia walimwogopa (mst. 5).*

9. Inamaana gani kwako kwamba Mungu ni mtakatifu ?

10. Je utajiweka hali gani mbele ya Mungu huyu mtakatifu sana?

## MARKO SURA YA 10

## ALIYE MKUU KULIKO WOTE KATIKA UFALME WA MUNGU (MARKO 10:32-45)

*Soma sura ya 10 yote ili uweze kuuelewa muktadha (mazingira). Halafu soma tena kuanzia mstari wa 32 mpaka wa 45. Mistari hii itakuwa ndiyo kiini cha somo hili.*

1. Kwa nini unafikiri wanafunzi walistaajabu na watu waliogopa? (mst. 32)

   1. Yesu alikwenda Yerusalemu ili akasulibiwe (mst. 32-34). Wanafunzi walimwambia Yesu afanye nini watakapokuwa naye katika utukufu? (mst. 35-37)

   2. Je, ilikuwa vibaya kwa Yakobo na Yohana kuuliza swali katika mstari wa 35? Kwa nini au kwa nini sio?

*'Kunyweni kikombe', 'ubatizo': Yesu alitumia taswira hizi kuzungumzia kifo chake. Atakinywea kikombe cha mateso cha ghadhabu ya Mungu. Atabatizwa katika hukumu ya Mungu.*

   3. Je wanafunzi wengine walijisikiaje waliposikia kile walichoomba Yakobo na Yohana? Kwa nini? (mst. 41)

   4. Ni jinsi gani Yesu anasema wanafunzi ni lazima wawe tofauti na watawala wa watu wa mataifa? (mst. 42-44)

6. Hii ni mara ya tatu (katika Marko) ambapo Yesu anazungumzia sababu za kuja kwake duniani. Linganisha: 1:38, 2:17 na 10:45. Ni zipi sababu hizo mbalimbali zilizomfanya Yesu aje?

*Fidia ni malipo yanayolipwa kwa kuwakomboa watumwa. Kama fidia imelipwa, mtumwa anapata uhuru wake. Hii ni picha ya Yesu akitoa maisha yake ili kutukomboa kutoka katika 'utumwa wa dhambi'. (Yohana 8:34)*

*Maswali ya kutafakari:*

7. Yesu anatoa mfano gani hapa?

8. Yesu alisema kwamba walio wakubwa kati ya watu wao ni wale ambao wanatumikiana kwa unyenyekevu. Ni jinsi gani unaweza kuwatumikia majirani na marafiki zako? Tafuta mifano mingine katika maisha ambapo unaweza kulazimika kuwaweka wengine mbele na kuwahudumia, kuliko kujifanyia mambo yako unayoyapenda tu.

9. Ina maana gani kwako kwamba Yesu alijitolea maisha yake yawe kama fidia? (mst.45)

## MARKO SURA YA 11

## KUINGIA YERUSALEMU (MARK 11:1-11)

*Soma sura ya 11 yote ili uweze kuuelewa muktadha (mazingira). Halafu soma tena kuanzia mstari wa 1 mpaka wa 11. Mistari hii itakuwa ndiyo kiini cha somo hili.*

1. Yesu na wanafunzi wake walikuwa wanakwenda wapi? (mst. 1)

2. Rejea sura ya 10:33-34. Yesu alisema kingetokea nini kule Yerusalemu?

3. Yesu aliwaambia wafanye nini katika kijiji kile? (mst. 2)

4. Wanafunzi walitakiwa kujibu nini iwapo mtu yeyote angewauliza? (mst. 3)

5. Watu walitandaza nini njiani? (mst. 8)

6. Watu walikuwa wakisema nini juu ya Yesu? (mst. 9-10)

7. Kwa nini unafikiri walikuwa wanasema hivyo kuhusu Yesu?

*Zaidi ya miaka 500 kabla ya kuja kwa Yesu, nabii wa Mungu Zekaria alinena kuhusu tukio hilo. (Zekaria 9:9)*

*Watu waliodhani kuwa Yesu alikuwa Masiha walitaka Yesu afanye ufalme wa kiduniani na awakomboe kutoka utawala wa Warumi. Kwa hiyo, hiyo ndiyo sababu watu walipaaza sauti na kuimba kusherehekea mfalme wao mpya. Hawakutambua kwamba ufalme wa Masiha haukuwa wa hapa duniani.*

*Maswali ya kutafakari:*

8. Ufalme wa Yesu si wa ulimwengu huu. Jaribu kuelezea ufalme wake ni wa namna gani?

9. Je, ni kwa namna gani Yesu ni mfalme wako? Hii inaathiri vipi maisha yako (maisha ya familia yako, kanisa lako, mji wako, kabila lako na taifa lako)?

## MARKO SURA YA 12

## AMRI KUU (MARKO 12:28-34)

*Soma sura ya 12 yote ili uweze kuuelewa muktadha (mazingira). Halafu soma tena kuanzia mstari wa 28 mpaka wa 34. Mistari hii itakuwa ndiyo kiini cha somo hili.*

1. Katika sura hii, tunasoma kuhusu watu kadhaa ambao walimpinga Yesu na walijaribu kumtega Yesu katika maneno yake. Kisha mwandishi wa sheria anakuja kwa Yesu. Waandishi walikuwa ni wataalamu katika mambo ya sheria ya Agano la Kale. Mwandishi alitambua kuwa majibu ya Yesu yalikuwa mazuri kabisa. Kisha akamwuliza Yesu swali. Je, mwandishi alimwuliza nini Yesu? (mst. 28)

2. Katika kujibu swali Yesu alinukuu kifungu kutoka Torati ya Musa katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Kilikuwa kitu gani? (12:29-30)

3. Amri hii ina maana gani?

4. Kisha Yesu akaongeza sehemu ya pili katika jibu lake ambalo linatoka katika kitabu cha Mambo ya Walawi. Yesu aliitaja amri gani kuwa ndiyo amri kuu ya pili? (mst.31)

5. Amri hii ina maana gani?

6. Kisha mwandishi alirudia jibu la Yesu. Baada ya kumsikiliza mwandishi, Yesu alimwambia nini? (mst. 34)

7. Maandiko yanasema kuwa baada ya Mafarisayo na Maherodi na Masadukayo kumkabili Yesu, hivyo hakuna mtu aliyejitokeza kumwuliza Yesu maswali mengine (mst. 34). Kwa nini unafikiri hawakumwuliza Yesu maswali mengine ya mtego?

*Maswali ya kutafakari:*

8. Unadhani amri ya kumpenda Mungu kuliko vitu vyote ndiyo ngumu kuliko zote? Kwa nini?

9. Ni namna gani unaweza kuishi maisha ambayo Yesu anakutaka uishi dhidi ya jirani yako?

## MARKO SURA YA 13

## YESU ATARUDI TENA (MARKO 13:24-37)

*Soma sura ya 13 yote ili uweze kuuelewa muktadha (mazingira). Halafu soma tena kuanzia mstari wa 24 mpaka wa 37. Mistari hii itakuwa ndiyo kiini cha somo hili.*

1. Katika mstari wa 24 Yesu ananukuu tena kutoka manabii wa Agano la Kale. Vitu gani ambavyo anasema vitatokea baada ya kipindi cha dhiki? (mst.24-26)

2. Wakati huo, Mwana wa Adamu atawatuma malaika wake kufanya nini? (mst. 27)

3. Kisha Yesu anatumia mti katika kuelezea mfano. Ishara ilikuwa nini katika mti ambapo unaonesha wakati wa mavuno umekaribia? (mst. 28)

4. Mfano huu una maana gani? (mst. 29)

*Kama vile majani mapya ya mtini yaashiriavyo kukaribia kwa msimu mpya wa masika, vivyo hivyo, dhiki ambazo Yesu alizielezea zinaashiria kwamba ujio wake wa pili umekaribia.*

5. Kitu gani kitapita kufuatana na mstari wa 31?

6. Ni nani pekee anayejua siku ya kurudi tena kwa Yesu?

7. Kisha Yesu akalinganisha kurudi kwa Kristo na kitu gani katika mstari wa 34 na 35?

8. Nini maana ya “akawakuta mmelala”? (mst. 36)

9. Kitu gani Yesu alisema kwa mara ya tano katika mstari wa 37? (Rejea mistari hii 9, 23, 33, 35)

*Maswali ya kutafakari:*

10. Yesu anajaribu kuwaeleza wanafunzi wake umuhimu wa kuwa tayari kwa ujio wake, pia kujishughulisha kuhusu ufalme wake wakati wakisubiri kurudi kwake. Ni namna gani unaweza kuwa tayari kwa kurudi kwake?

11. Ina maana gani kwako kujishughulisha na ufalme wake?

## MARKO SURA YA 14

## KARAMU YA BWANA (MARKO 14:17-26)

*Soma sura ya 14 yote ili uweze kuuelewa muktadha (mazingira). Halafu soma tena kuanzia mstari wa 17 mpaka wa 26. Mistari hii itakuwa ndiyo kiini cha somo hili.*

1. Weka matukio yaliyoelezewa ndani ya sura hii katika mpangilio unaotakiwa: Yesu mbele ya baraza – Usaliti wa Yuda – Petro anamkana Yesu – Kukamatwa kwa Yesu – Yesu anapakwa mafuta Bethania – Yesu anasali Gethsemane – Yesu anakula karamu ya mwisho pamoja na wanafunzi wake.

2. Walipokuwa wakila, Yesu aliwaambia nini wanafunzi wake? (mst.18)

3. Hakuna hata mmoja wa wanafunzi aliyefikiri kuwa mmoja wao angemsaliti Yesu. Kitu gani walisema kila mmoja wao? (mst. 19)

4. Yesu alimtambulisha msaliti wake kwa vitu gani viwili? (mst. 20)

5. Kisha Yesu akachukua mkate na akamshukuru Mungu. Halafu, alifanya nini na ule mkate? Je, alisema nini? (mst. 22)

6. Unafikiri Yesu ana maana gani anaposema mkate ule ni mwili wake mwenyewe? Tazama pia Yohana 6:47-48.

*Yesu alikuwa karibu kutoa mwili na damu yake kama sadaka kwa wanadamu kwa ajili ya msamaha wa dhambi. Sadaka ya Yesu ya mara moja, iliweza kulipa adhabu ya dhambi zetu milele. Damu yake ilimwagika kwa utakaso wa dhambi za wanadamu.*

7. Kisha Yesu akachukua kikombe, akashukuru, akawapa wanafunzi wake. Alisema nini alipokuwa akiwapa? Nao (wanafunzi) walifanya nini nacho? (mst. 24) Maneno yake yalikuwa na maana gani?

8. Katika mstari wa 25, Yesu alisisitiza jambo. Lilikuwa jambo gani?

*Maswali ya kutafakari:*

9. Karamu ya Bwana maana yake nini ?

10. Je wewe hushiriki katika Karamu ya Bwana? Kwa nini siyo au ndiyo? Kama ndiyo, ina maana gani kwako? Kama siyo, unaweza kutafuta njia ya kutatua tatizo hili?

## MARKO SURA YA 15

## KUSULIBIWA KWA YESU (MARKO 15)

*Soma sura yote ya 15.*

1. Yesu alikamatwa na kupelekwa mbele ya kuhani mkuu na Pilato. Wayahudi walipiga kelele wakitaka Yesu auawe, na Pilato akamkabidhi Yesu mikononi mwa Wayahudi. Askari walimpiga Yesu kwa mijeredi na kumdhihaki. Walimpeleka wapi baada ya pale? (mst.20)

2. Ni nani aliyelazimishwa kubeba msalaba wa Yesu na askari wa Kirumi? (mst. 21) Kwa nini unafikiri mtu mwingine angetakiwa kuubeba msalaba wa Yesu?

3. Askari wa Kirumi walifanyia nini mavazi ya Yesu? (mst. 24)

4. Nani pia alisulibiwa pamoja na Yesu? (mst. 27)

5. Watu waliokuwa wakipita njiani walimfanyaje Yesu wakisema nini? (mst. 29-30)

6. Makuhani wakuu na waandishi walikuwa wakisema nini ili kumdhihaki Yesu? (mst. 31-32)

7. Kisha, katika mstari wa 33, kitu gani kilitokea? Ilikuwa saa ngapi mchana?

8. Yesu alisema nini? (mst. 34) Kwa nini unafikiri kuwa Yesu alisema haya?

*Yesu alikuwa amebeba kila dhambi ya watu wote wa ulimwengu. Dhambi zinamtenga mtu na Mungu. Hiyo nidyo maana Yesu alijisikia kuachwa na Mungu kwa sababu alikuwa ametengwa na Mungu wakati alipokuwa msalabani. (Tazama pia 2 Kor. 5:21 na Wagalatia 3)*

9. Kilitokea nini hekaluni mara Yesu alipokata roho? (,mst.37-38)

*Katika hekalu ambamo Wayahudi waliabudu, kulikuwa na chumba maalumu cha ndani kilichoitwa “mahali patakatifu” ambapo Mungu alikuwepo katika namna tofauti. Mahali patakatifu siku zote palikuwa pamefichwa mbali na watu na makuhani kwa pazia kubwa. Ni kuhani mkuu pekee ndiye aliyeruhusiwa kupita pazia hilo kwenda mahali patakatifu mara moja kwa mwaka kukutana na Mungu akiwa na sadaka ili kuomba msamaha wa dhambi za watu.*

*Lakini Yesu alipomwaga damu yake na kufa, yeye alikuwa ndiye sadaka ya mwisho ya kulipia dhambi zote za watu. Yeye akawa ndiye Kuhani mkuu milele yote. Akawa ndiye mpatanishi pekee kati ya Mungu na wanadamu. (1Tim 2:5). Ndio maana Mungu alipasua pazia lile kubwa katika hekalu wakati Yesu alipokufa –ili kutuonesha wazi wazi kuwa sasa, kupitia Yesu tuwe na fursa ya moja kwa moja kuingia kwa Mungu.*

*Maswali ya kutafakari:*

10. Yesu alidharauliwa na kunyanyaswa na kuteswa katika mikono ya watu wenye dhambi ambao walikataa kuwa Yesu ni Masiha na ni mwana wa Mungu. Ni kwa nini ilimpasa Yesu afe? Kuna nini kibaya kuhusu dhambi yako na yangu?

11. Ni nini kimebadilika kutokana na kifo chake? Kifo chake kina maana gani kwako?

## MARKO SURA YA 16

## KUFUFUKA KWA YESU (MARKO 16)

*Soma sura yote ya 16.*

1. Yesu alikuwa ameshakufa na kuzikwa kaburini. Utabirii wake katika Marko 8:31, 9:31 na 10:33-34 umekuwa umetimia dhahiri. Soma tena vifungu hivi vitatu. Ni kifungu gani cha mwisho kati ya vifungu vyote vitatu vya utabiri?

2. Nani walikuja kwenye kaburi la Yesu? (mst. 1) Wanawake hawa walikuwa wanapanga kufanya nini?

3. Ilikuwa saa ngapi mchana? (mst.2)

*Ilikuwa siku ya kwanza ya juma ya wiki ya kiyahudi, ambayo ilikuwa ni Jumapili.*

4. Walipokuwa wakitembea, walikuwa wana hofu juu ya kitu gani? (mst. 3) Badala yake waliona nini? (mst. 4)

5. Wanawake wakaingia katika kaburi lililo wazi. Walipokuwa wakiingia waliona nini? (mst. 5) Walifanya nini?

6. Mtu aliyekuwa katika vazi jeupe aliongea nao. Sema kwa maneno yako mwenyewe maneno aliyosema malaika. (mst. 6)

7. Kisha wanawake walifanya nini? (mst. 8)

*Kwa sababu Yesu alizikwa haraka haraka kabla ya Sabato kuanza, hakukuwa na muda wa kupaka manukato mwili wake. Ndio maana wanawake wale watatu walitaka kufanya hivyo haraka iwezekanavyo mara baada ya Sabato kwisha.*

8. Kwa nini kuna umuhimu sawa kabisa kati ya kusulubiwa na kufufuka kwa Yesu?

9. Yesu yuko wapi sasa? (mst. 19)

*Maswali ya kutafakari: Tumia muda kidogo kufikiri na kujiuliza kuhusu maswali haya wewe binafsi na katika vikundi. Mwombe Mungu akusaidie.*

10. Ni amri gani ya mwisho ya Yesu ambayo Marko anaielezea katika Injili yake? Hii ina maana gani? Kwa namna gani tuiishi amri hiyo?